*Kioo cha Lugha, Juz. 23(2), 277-295*
*Jarida la Taasisi ya Taaluma za Kiswahili*
*Chuo Kikuu cha Dar es Salaam* DOI: https://dx.doi.org/10.4314/kcl.v23i2.7

# Taswira za Bahari katika Riwaya ya *Uhuru wa Watumwa* (1934)

*Shani O. Mchepange*[1] *na Grace H. Minja*[2]

## Ikisiri

Simulizi za watumwa zinapatikana katika vyanzo mbalimbali, ikiwa ni pamoja na riwaya ya James Mbotela iitwayo *Uhuru wa Watumwa* (1934), ambayo imesheheni nduni anuwai za kifani na kimaudhui. Miongoni mwa nduni hizo ni taswira za bahari. Taswira za bahari hutumiwa na wasimulizi au waandishi ili kuwasilisha ujumbe uliokusudiwa. Makala hii inajadili taswira za bahari katika riwaya ya *Uhuru wa Watumwa* pamoja na dhima zake. Riwaya hii imeteuliwa kwa makusudi kwa sababu ndiyo riwaya pekee ya Kiswahili inayozungumzia utumwa kwa kina. Makala imeongozwa na Nadharia ya Udenguzi ya Jacques Derrida. Data zimekusanywa kwa kufanya usomaji makini wa riwaya hiyo. Matokeo yanaonesha kwamba riwaya hii imeichora bahari katika taswira mbalimbali. Baadhi ya taswira hizo zinakinzana lakini zinajengana na zinakamilishana katika simulizi husika. Miongoni mwake ni bahari kuashiria usalama na pia hatari au kifo, bahari kuashiria uhuru na utumwa, bahari kuashiria muungano na utengano, na kadhalika. Vilevile, zipo taswira za bahari ambazo hazioneshi jozi zenye ukinzani. Makala imebaini dhima kadhaa zinazotokana na kutumia taswira za bahari. Baadhi ya dhima hizo ni kuonesha athari za biashara ya watumwa, kubaini mchango wa watumwa katika maendeleo ya uchumi duniani, kujenga uelewa wa msomaji kuhusu biashara ya watumwa, kuibua hisia kwa msomaji, na kusawiri mandhari ya biashara ya watumwa.

## 1.0 Utangulizi

Simulizi za watumwa, kama utanzu wa fasihi, zina utajiri mkubwa wa fani na maudhui yake. Miongoni mwa utajiri huo kwa upande wa fani ni ruwaza yake, motifu zinazojitokeza, lugha inayotumika na taswira mbalimbali. Makala hii inajadili taswira zinazoibuliwa na bahari katika simulizi za watumwa pamoja na dhima zake. Tumechunguza taswira za bahari kwa sababu bahari ilikuwa ndiyo njia kuu ya kusafirisha watumwa kutoka Afrika kwenda sehemu mbalimbali duniani wakati wa biashara ya watumwa. Taswira ni kipengele cha lugha. Mulokozi (2017) anafasili taswira kama mbinu ya kuumba picha ya jambo katika utungo na katika

[1] Profesa Mshiriki, Taasisi ya Taaluma za Kiswahili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Tanzania. Baruapepe: shaniom@yahoo.co.uk
[2] Mhadhiri, Taasisi ya Taaluma za Kiswahili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Tanzania. Baruapepe: gracehenryminja@gmail.com

mawazo ya msomaji au msikilizaji wa utungo huo kwa kutumia maneno. Naye Wamitila (2008) anaeleza kwamba taswira zinaweza kuwa za kimaelezo (zinazoundwa kutokana na maelezo au uteuzi wa maneno tu) au zikawa za kiishara (maneno au maelezo yenye uwezo wa kuashiria kitu kingine, yaani yana ujumbe wa ziada). Vilevile, kuna taswira nyingine mbalimbali zikiwamo zile za kuona, za mawazo na za hisi (Njogu na Chimerah, 1999). Kazi ambayo imechunguzwa katika makala hii ni riwaya ya *Uhuru wa Watumwa* (1934). Riwaya hii ya kihistoria ni simulizi ya mwanzo na pekee ya Kiswahili kuhusu utumwa na biashara ya watumwa katika Afrika Mashariki (Khamis, 2005). Kwa hiyo, imetusaidia kupata data stahiki.

Biashara ya watumwa na simulizi za watumwa kama kazi za fasihi zimetafitiwa na wataalamu mbalimbali kihistoria na kifasihi. Miongoni mwa tafiti za kihistoria kuhusu biashara ya watumwa kupitia bahari ya Hindi, Atlantiki, Mediterania na bahari ya Shamu ni zile za Cooper (1977), Patterson (1982), Sheriff (1987), Lovejoy (1989), Liebst (2023), Pargas na Schiel (2023) na Thiebaut (2025). Mathalani, Cooper (1977) anazungumzia utumwa wa mashambani katika pwani ya Afrika Mashariki katika maeneo ya Zanzibar, Pemba, Mombasa na Malindi katika karne ya 19 na athari zake kwa watumwa. Aidha, analinganisha utumwa katika maeneo hayo na ule unaopatikana katika sehemu nyingine za Afrika na Amerika. Sheriff (1987) anazungumzia kuhusu utumwa katika bahari ya Hindi, hususan visiwani Zanzibar na pwani ya Afrika Mashariki. Anaeleza kwamba Zanzibar ilikuwa kituo kikubwa cha biashara ya watumwa Afrika Mashariki wakati wa utawala wa Sultani wa Oman kati ya miaka ya 1770 hadi 1873. Biashara ya watumwa, karafuu na pembe za ndovu iliunganisha bara, visiwa na bahari ya Hindi na kuchangia kwa kiasi kikubwa katika uchumi wa Uarabuni, India na Ulaya. Hivyo, biashara ya watumwa ilikuwa na athari chanya na hasi kwani haikuwa tu ukatili bali pia sehemu ya uhusiano mpana wa kiuchumi duniani. Aidha, Sheriff anaeleza kwamba watumwa walikuwa si tu biashara bali pia walitumika kama nguvukazi katika kilimo cha karafuu ambacho kilikuwa nguzo muhimu ya uchumi wa Zanzibar.

Baadhi ya tafiti hizo za kihistoria zimezungumzia athari za kijamii na kiuchumi za utumwa, ikiwamo kifo cha kijamii na kiutamaduni kwa watumwa, kutokana na kutengana na familia na koo zao (Patterson, 1982), kupungua kwa idadi ya watu katika bara la Afrika, ubaguzi wa rangi na mabadiliko ya utambulisho (Lovejoy, 1989; Pargas na Schiel, 2023). Vilevile, biashara ya watumwa katika Afrika Mashariki kunako karne ya 19 hadi mwanzoni mwa karne ya 20, imechangia katika maendeleo ya miji kama Zanzibar, Mombasa na Lamu (Sheriff, 1987; Liebst, 2023). Aidha, Thiebaut (2025) amechunguza kushamiri kwa biashara ya watumwa katika bahari ya Hindi katika nchi za Afrika Mashariki kama vile Somalia, Madagascar, Msumbiji, Komoro na pwani ya Waswahili. Amelinganisha biashara ya watumwa katika bahari ya Hindi na bahari ya Atlantiki, na kubaini tofauti kadhaa, ikiwamo ile ya bahari ya Hindi kudumu zaidi kuliko ile ya Atlantiki. Kimsingi, kazi hizi za kihistoria zimejenga uelewa wetu kuhusu biashara ya watumwa kupitia

maeneo mbalimbali na mchango au athari yake kwa jamii. Hivyo, zimetupa mwanga katika uchambuzi wa data za makala hii kuhusu taswira za bahari na dhima zake.

Kwa upande wa tafiti za kifasihi, kuna tafiti kama zile za Baderoon (2009), Murphy (2012), Campbell (2012), Beach (2013) na Henry (2020). Mathalani, Baderoon (2009) alichunguza bahari za Afrika kama kumbukumbu ya utumwa katika fasihi na utamaduni wa Afrika Kusini. Utafiti wake ulibaini kwamba bahari ni eneo lenye kumbukumbu na mateso kwa watumwa. Pia, biashara ya watumwa na mizunguko ya bahari iliyounganisha Afrika, Ulaya na Asia imesaidia kuleta utamaduni wa kisasa katika lugha, dini na vyakula, miongoni mwa watumwa na jamii. Kwa upande wake, Murphy (2012) alichunguza taswira ya biashara ya watumwa katika fasihi ya Afrika Magharibi. Alibaini kwamba kazi hizo zinapozungumzia mambo kama minyororo, maji na ardhi zinawakilisha maumivu, vifo, mateso, hofu na unyanyasaji, si tu kwa watumwa bali pia kwa wote waliobaki Afrika Magharibi na vizazi vyao. Naye Beach (2013) alichunguza simulizi za kihistoria za watumwa wa Waingereza nchini Morocco. Anaeleza kwamba simulizi hizo zinaonesha kuwa watumwa hao walitumika kama chombo cha kisiasa na kijeshi katika kujenga jeshi la watumwa wa Kiafrika katika kudumisha utawala wa Sultani wa Morocco. Watumwa hao walihudumu katika majeshi na familia za kifalme. Anaeleza zaidi kwamba simulizi hizi ziliongelea uhusiano wa kidini wa dini ya Kiislamu na Kikristo, utamaduni wa Kiislamu na siasa za Morocco. Pia, Henry (2020) alifanya utafiti linganishi kuhusu ujumi wa kifasihi katika simulizi teule za watumwa kutoka Afrika, Amerika na Ulaya. Utafiti wake ulibaini kuwa, ijapokuwa simulizi za watumwa ni utanzu mahususi wa kifasihi, kuna masuala anuwai yanayotofautisha simulizi za watumwa kutoka maeneo tofauti ya kijiografia, ikiwamo majina ya simulizi hizo, ruwaza na hata maudhui. Miongoni mwa mambo yanayosababisha tofauti hizo ni miktadha tofauti ya utunzi. Makala hii ya sasa ni mwendelezo wa tafiti za kifasihi kuhusu biashara ya watumwa, inayolenga kuangazia taswira za bahari katika fasihi ya Kiswahili katika pwani ya Afrika Mashariki.

## 2.0 Methodolojia ya Utafiti

Riwaya ya *Uhuru wa Watumwa* ni miongoni mwa riwaya za kihistoria za Kiswahili. Riwaya hii ni simulizi ya mwanzo na pekee kuhusu utumwa na biashara ya watumwa katika Afrika Mashariki (Khamis, 2005). James Juma Mbotela, mwandishi mwenye asili ya utumwa, anasimulia hadithi hii kuhusu uzoefu aliopitia baba yake katika utumwa, biashara iliyokuwa inafanywa na kumilikiwa na Waarabu, mnamo karne ya 17 na 19 katika Afrika Mashariki. Pia, anaeleza jitihada za Mwingereza katika kusitisha biashara ya watumwa kwa kuwakomboa Waafrika. Anasimulia kumbukumbu za baba yake kuhusu jinsi alivyokombolewa na Jeshi la Majini la Uingereza kutoka kwenye majahazi ya watumwa ya Kiarabu. Riwaya inaeleza mchakato wa kuwapata watumwa, kuwauza, shida na mateso waliyopata

na namna walivyokuwa wanakombolewa na Mwingereza na hatimaye kuanza maisha mapya.

Uteuzi wa riwaya hii umefanywa kwa kutumia mbinu ya usampulishaji lengwa (wa kimakusudi). Riwaya hii inahusiana moja kwa moja na mada ya utafiti wetu na ndiyo riwaya pekee ya Kiswahili inayozungumzia utumwa katika bahari ya Hindi kwa kina. Data za makala hii zimekusanywa kwa kusoma riwaya teule kwa kina ili kubaini taswira hizo. Usomaji huo ulifanyika kwa kumakinikia sehemu mbalimbali katika riwaya zinazozungumzia bahari moja kwa moja au kwa ishara. Sehemu na vipengele vilivyozingatiwa ni sentensi, sura, matukio mbalimbali katika utekelezaji wa biashara ya watumwa, kauli za wahusika, matendo ya wamiliki wa watumwa na watumwa na hali au hisia za wahusika/watumwa katika mandhari ya bahari. Kisha data zilichambuliwa kwa kuongozwa na Nadharia ya Udenguzi.

## 3.0 Nadharia ya Utafiti

Makala hii imeongozwa na Nadharia ya Udenguzi iliyoasisiwa na mwanafalsafa wa Kifaransa Jacques Derrida (1930-2004) mwishoni mwa miaka ya 1960 na mwanzoni mwa miaka ya 1970. Derrida anapinga mitazamo ya Kimagharibi ya kutazama mambo kwa namna mbili zinazokinzana na kuwapo kwa mipaka thabiti ya jozi za maneno kinzani au mawazo yanayopingana katika lugha kama vile dhana ya kuwapo/kutokuwapo, zuri/ovu na mwanaume/mwanamke. Anaona kwamba mipaka baina ya jozi kama hizi za maneno kinzani si imara au thabiti, kwani dhana hizi zinahusiana na kutegemeana. Derrida anapinga falsafa na tamaduni nyingi za Kimagharibi zinazoona kwamba jozi kinzani zina majukumu yanayokinzana na yasiyoweza kushirikiana. Pia, huona kwamba neno linalotajwa kwanza mara nyingi hupewa hadhi ya juu, chanya au hupendelewa kuliko jingine. Pande hizi mbili huonekana kuwa tofauti kabisa na hazina mwingiliano. Hivyo, msingi wa kwanza wa nadharia hii kwa mujibu wa Derrida unadadisi jozi kinzani na unaona kwamba kila neno katika jozi haliwezi kueleweka peke yake bali maneno yanahusiana, kwani kila neno hutegemea kuwapo kwa lenzake ili kupata maana (Derrida, 1967, 1972).

Msingi wa pili wa nadharia hii ni kwamba kuna maana na tafsiri nyingi zinazojitokeza katika lugha. Hivyo, nadharia hii inapinga wazo kwamba kuna maana thabiti, kamili au ya kudumu na badala yake inaona kuwa maana ni ya kubadilika na daima iko wazi kwa marekebisho. Hivyo, lugha haina tafsiri kamili au ya mwisho kwani maana haina mwisho na tafsiri yake haina mwisho. Msingi wa tatu wa nadharia hii ni kwamba msomaji wa matini ana nafasi muhimu katika kujenga maana, kwani tafsiri hutegemea miktadha mbalimbali na ni za kibinafsi[3]. Hivyo, matini hupaswa kusomwa kwa undani zaidi ili kupata maana ya ndani. Msingi wa nne wa nadharia hii ni ule unaosisitiza kwamba kazi ya mtu binafsi si kazi iliyojitosheleza yenyewe, bali ni zao la uhusiano na maandiko mengine – ya kifasihi

---

3 "Deconstruction Literary Theory" https://english-studies.net/deconstruction-literary-theory/ imesomwa tarehe 15, Agosti 2025.

na yasiyo ya kifasihi (Derrida, 1972). Nadharia hii imewezesha kubaini na kufasiri taswira mbalimbali za bahari zilizotumika katika riwaya hii. Mathalani, kwa kutumia msingi wa kwanza taswira kinzani zimeoneshwa namna zinavyokamilishana katika kusawiri mada husika. Pia, kwa kutumia msingi wa pili na wa tatu, nadharia hii imetupa fursa nzuri ya kufasiri taswira za bahari kwa kuhusisha mjadala wetu na dhana nyingine zinazohusiana na bahari kama vile pwani, bandari, majahazi, maji, mawimbi, ufuko, mikoko, dhoruba za mawimbi na upepo ili kufafanua na kujenga maana ya taswira ya bahari. Vilevile, kwa kutumia msingi wa pili hadi wa nne, tumejadili taswira nyingine mbalimbali kwani maana au tafsiri ya kitu haina ukomo na hutegemea muktadha na viashiria vingine mbalimbali vya lugha. Vilevile, imesaidia kubaini dhima za taswira hizo. Sehemu inayofuata inahusu uchambuzi wa taswira za bahari katika riwaya teule.

## 4.0 Taswira za Bahari katika *Uhuru wa Watumwa*

Katika riwaya hii, bahari ya kawaida imetumika kama mojawapo ya miundombinu ya usafiri na kama sehemu ya kufanya shughuli au kupata mahitaji mbalimbali ya kijamii. Miundombinu hii inaonekana kutumika na vyombo vya Waarabu kama vile majahazi na Waingereza kama vile meli na manowari. Aidha, watumwa wengi wa Afrika Mashariki na Kati, baada ya kusafiri mwendo mrefu kwa miguu kutoka bara au maeneo ya asili/nchi zao, walisafirishwa kwa njia ya bahari. Usafiri huu wa bahari ndio uliwapeleka watumwa katika nchi mbalimbali kama vile Uarabuni, India na kwingineko ili kutumikishwa. Vilevile, ulitumika kuwaleta Waarabu kuja kuchukua watumwa Afrika Mashariki. Martin na Ryan (1977) wanakadiria kwamba kati ya mwaka 1780 na 1896 watumwa wapatao 424,100 kutoka Afrika ya Mashariki walisafirishwa kwa meli kwenda Uarabuni, Iran na India. Watumwa takriban 833,000 walibaki katika pwani ya Afrika ya Mashariki wakifanya kazi kwenye mashamba makubwa na katika kaya za tabaka la juu. Naye Austen (1989), kama alivyonukuliwa na Kusimba (2004: 65), anaeleza "Katika karne ya kumi na tisa pekee, watu 313,000 kutoka pwani za Kenya na Tanzania walisafirishwa kwa meli kwenda katika nchi hizo hizo".

Kwa upande wa bahari kama sehemu ya kufanyia shughuli au kupatia mahitaji mbalimbali ya kijamii, riwaya inaonesha bahari ikitumika kwa shughuli kama kuoga, kuvuna mikoko na kupata chakula (samaki). Mathalani, inaelezwa kuwa, "Watoto wengi walikuwa wakioga katika pwani ya amani ya Kisauni; kando ya majahazi ya Waarabu yaliyokuwa yamepakia fito za mikoko katika pwani hii" (uk. 59). Aidha, Juma na baba yake walikuwa wanaongelea na kulinganisha samaki wa Mpanda (bara ambako hakuna bahari) na samaki wa pwani. Hapa dhana ya pwani tunaichukulia kama bahari. Kwa kuwa palipo na pwani kuna bahari na hivyo mipaka baina ya dhana hizi si thabiti.

Data zetu zinaonesha kwamba bahari inawakilisha taswira mbalimbali na baadhi ya taswira hizo zinajenguana na kujengana. Kwa mfano, bahari inaashiria wokovu pia kifo, bahari inaashiria uhuru pia utumwa, bahari inaashiria muungano

pia utengano, bahari inaashiria amani pia mateso, na kadhalika. Taswira hizi zinajengana na kukamilishana katika kujenga simulizi nzima. Mbali na taswira hizo zenye ukinzani, zipo pia taswira nyingine kadhaa na mjadala wake ni kama ifuatavyo:

### 4.1 Bahari kama Ishara ya Utumwa

Utumwa ni hali au aina ya utegemezi wa kijamii na kiuchumi ambapo mtu mmoja anakuwa na mamlaka kamili ya maisha, kazi na uhuru wa mtu mwingine (Lovejoy, 2000). Biashara ya watumwa ilifanyika kwa watumwa kusafirishwa kupitia bahari. Bahari kama vile ya Hindi na Atlantiki zilikuwa njia kuu ya biashara ya watumwa kutoka Afrika kuelekea Uarabuni na sehemu nyingine duniani kama vile Asia, Ulaya na Amerika. Utumwa wa kimataifa ulitegemea bahari kupitia vyombo vya usafirishaji kama vile meli na majahazi kama njia kuu ya kusafirisha watumwa, kuunganisha masoko yao na kukuza uchumi wao (Lovejoy, 1989; Pargas na Schiel, 2023). Katika riwaya teule inaoneshwa namna Waarabu walivyotumia bahari kuwa njia ya biashara hiyo ya watumwa na kukuza masilahi yao. Bandarini ndipo palikuwa sehemu ya kuuzia watumwa hao. Martin na Ryan (1977) na Austen (1989) wanaeleza kwamba watumwa kutoka Afrika Mashariki ama walisafirishwa kwa meli kwenda Uarabuni, Iran na India au walibaki katika pwani ya Afrika Mashariki wakifanya kazi kwenye mashamba makubwa na katika kaya za watu wa tabaka la juu.

Watumwa walipofika baharini (bandarini) walijua kwamba sasa safari yao ‘rasmi’ ya kuuzwa imetimia. Watumwa wengine waliuzwa kutumika ndani ya nchi au kwenda nje ya nchi kwa kusafirishwa kwa vyombo vya usafiri vya baharini. Kwa kupanda vyombo hivyo, waliamini kwamba wameachana na nchi yao na wameenda kuanza maisha mapya ya kufanya kazi za kitumwa katika nchi za mbali. Inasimuliwa kwamba kwa watumwa “Pwani hiyo ilikuwa ya huzuni kwa kweli! …” (uk. 30). Ni sawa na kusema kwamba pwani ilikuwa sehemu ambayo huwezi kurudi nyuma tena. Mazungumzo ya watumwa, Mzee Mponda kwa Mzee Mambo, yanadhihirisha hili, “Basi baada ya siku chache, sisi sote tulitelemshwa[4] pwani mpaka bandari hiyo iliyokuwa ya kuuzwa watumwa. Tukijua kufungwa vitambaa vya macho na kuongozwa majahazini vilevile na pingu zetu za shingo” (uk. 43). Kwa kutumia Nadharia ya Udenguzi inayomtaka msomaji kusoma matini na kutafakari kwa kina ili kuipata maana au fasili ya ndani, tunaona kwamba kutokana na biashara ya watumwa kufanyikia pwani/bandarini na majahazi ya kuwasafirisha kuwapo hapo na kuwasafirisha, bahari inaashiria utumwa. Bahari ilitumika na kuwakilisha safari nzima ya kutoka Afrika Mashariki kuelekea huko utumwani.

[4] Neno hili limeandikwa hivi kitabuni.

**4.2 Bahari Inaashiria Kutengana na Familia na Utamaduni Asilia**

Biashara ya watumwa ilifanya wazazi kutengana na watoto wao na waume kutengana na wake zao. Mbali na utengano, athari nyingine kama zinavyoelezwa na tafiti mbalimbali ni kupungua kwa idadi ya watu katika bara la Afrika, ubaguzi wa rangi na utambulisho mpya (Lovejoy, 1989; Pargas na Schiel, 2023). Familia nyingi zilivunjika kwa kuwa watumwa walikuwa wakitumikishwa katika maeneo mbalimbali, mbali na nyumbani. Watumwa walipofika pwani wakitokea bara, waliuzwa kwa wamiliki tofauti na walipakiwa katika vyombo tofauti kutokana na kwamba kila mmiliki alikuwa na vyombo vyake vya kupakia watumwa wake. Inasimuliwa katika riwaya kwamba utaratibu uliokuwa unatumika na wafanyabiashara wa watumwa wakiona watumwa ni wengi na "hawataweza kuingia wote katika majahazi" yao, wengine waliuzwa hapo "bandarini kwa Waarabu wengine" na wengine walikwenda "Bara Arabu" (uk. 28). Ama kwa kuuzwa na kubaki Afrika Mashariki au kwenda nje ya Afrika Mashariki, watumwa wengine hawakuwahi kuonana tena maishani mwao. Hivyo, baada ya watumwa kufikishwa baharini inasimuliwa kwamba, "Pwani hiyo ilikuwa ya huzuni kweli! Mama alikuwa akitengwa na mwanawe na mama akitengwa na baba. Kina mama walikuwa wakilia sana kwa sababu watoto wao walikuwa wakiuzwa mbali nao" (uk. 30). Utengano huu si tu unaleta huzuni bali ni kuanza kwa maisha mapya ya bila ya kuwa na wapendwa wao, yaani kutengana.

Kwa upande wa utamaduni, watumwa walipofika huko waliweza kuendeleza baadhi ya vipengele vya tamaduni zao kama vile mila, dini na ibada, hadithi, ushairi, muziki na lugha za Kiafrika. Hata hivyo, kwa kiasi kikubwa walipoteza utambulisho wao wa kikabila na kujikuta wakilazimishwa kufuata mila, dini na lugha za wamiliki wao au kufuata utamaduni mseto (Patterson, 1982; Gilroy, 1993; Lovejoy, 2000). Utamaduni huo ulichanganya vipengele vya utamaduni wa Afrika, Ulaya, Uarabuni na Amerika, kutegemeana na sehemu walipokuwa wanatumikia utumwa huo. Hivyo, safari za majini kwa watumwa zilikuwa ishara ya kuachana na mila zao, desturi zao, tamaduni zao, vyakula na kadhalika. Watumwa walipofika katika maeneo walikokuwa wanapelekwa kwa ajili ya kufanyishwa kazi za kitumwa, walianza maisha na utamaduni mpya. Inasimuliwa katika riwaya kwamba, Mtipia, mmojawapo wa watu waliokamatwa ili wauzwe kama watumwa, hakupendezewa na safari hiyo akawaambia wenziwe, "Mimi nitatoroka usiku huu. Ni radhi kuuzwa mtumwa katika hii nchi yetu lakini sikubali kuvuka bahari na kupelekwa Bara Arabu" (uk. 28). Kwa kuongozwa na Nadharia ya Udenguzi inayomwezesha msomaji kufanya fasiri ya matini kwa undani kulingana na muktadha husika, maneno haya yanaweza kumaanisha kwamba ni afadhali kubaki nyumbani (Afrika Mashariki) kuliko kwenda mbali ambako mtu huwa mgeni kabisa wa watu, utamaduni na mazingira. Suala la watumwa kutotaka kutoka katika maeneo yao ya asili ili kwenda kutumikishwa katika maeneo mengine tofauti linasawiriwa vyema katika simulizi mbalimbali za watumwa na bunilizi za fasihi ya watumwa. Miongoni mwazo ni *The Interesting Narrative of Olaudah Equiano or*

*Gustavus Vassa: The African* (1789), *Tendehogo* (1984) na *Mama Meli: From Slavery to Freedom* (1993).

Vilevile, inasimuliwa kwamba, kwa upande wa chakula, watumwa waliookolewa na Mwingereza mle baharini, walianza kula nyama ya nguruwe. Chakula hicho kiliwapendeza kutokana na utamu wake. Pia, walianza kuoga maji ya bomba, waliyoyaita 'nyoka mkubwa'. Walianza kwa kuogopa sana na wengine kutumbukia baharini kwa woga uliosababisha baadhi yao kufa. Hata hivyo, mwishowe walizoea. Aidha, walifundishwa kupiga ngoma ya "bendi" (uk. 38). Halikadhalika, watumwa waliookolewa waliwekewa walimu Wazungu wa dini ili kuwafunza Injili, "wajue mapenzi ya Mungu wa kweli wasiyemjua wala kumsikia" (uk. 41). Kwa ujumla, tamaduni za kigeni zilichangia kudhoofisha tamaduni za asili za watumwa kwa sababu walilazimika kujifunza tamaduni mpya na kuacha lugha, mila na imani zao (kama vile vyakula, dini, sanaa) ili kuendana na mfumo mpya wa watawala. Kwa mantiki hiyo, walijikuta wakifuata na kujitambulisha kwa tamaduni za kigeni kuliko zao za asili. Akiongelea athari ya utumwa katika Afrika Kusini, Baderoon (2009) anaeleza pia kwamba Bahari ya Hindi ni eneo muhimu lililosaidia watumwa kuweza kujifunza utamaduni wa kisasa kama vile lugha, dini na chakula. Kwa kutumia Nadharia ya Udenguzi inayomwezesha mchambuzi kufasiri matini kwa kina ili kubaini maana mbalimbali zilizojificha, tunaona kwamba mifano hii tuliyoidondoa katika sehemu hii inawakilisha vizuri taswira ya bahari kama utengano na jamii yao pamoja na utamaduni wao na kuanza mtagusano na jamii na utamaduni mwingine.

**4.3 Bahari Inawakilisha Hatari, Misukosuko, Mateso na Ukatili**

Riwaya ya *Uhuru wa Watumwa* inaichora bahari kama sehemu hatari na iliyojaa misukosuko, mateso na ukatili. Watumwa walipoingia katika majahazi ya Waarabu kuelekea Uarabuni walikabiliana na safari ndefu yenye hatari na misukosuko ya bahari yenyewe pamoja na mateso na ukatili kutoka kwa wamiliki wao. Watumwa wakiwa safarini walishikwa na njaa, kiu, uchovu, magonjwa, maumivu na kukosekana kwa utu. Wengine walitafakari hatari ya safari hiyo au maisha ya mateso na ukatili ambao wangeenda kufanyiwa wafikapo utumwani. Hivyo, baadhi yao waliamua kujitosa majini na kufia huko kuliko kukabiliana na hali ya hatari, mateso na ukatili walioupata kutoka kwa Waarabu wakiwa humo safarini au huko waendako. Tafiti kuhusu utumwa zinaonesha namna watumwa walipokuwa safarini katika meli na majahazi walivyokumbwa na uhaba wa chakula na maji, na mateso na ukatili kiasi cha kuleta uasi na hata kutoroka (taz. Patterson, 1982; Lovejoy, 2000; Campbell, 2012). Mathalani, inasimuliwa kwamba shehena za majahazi zilizojaa watumwa zilipokuwa zinatoka bandarini watumwa waliona "safari hii ya kutisha… Hawakuthubutu kuyaangalia maji, kwa sababu walikuwa wakishikwa na kizunguzungu, wakitapikiana ovyo tu katika majahazi" (uk. 30).

Aidha, hatari ya safari hiyo ya majini ilitokana na misukusuko kadha wa kadha kama vile chombo kuharibika, hali mbaya ya hewa, safari kuwa ndefu na

mashetani wa baharini. Mathalani, inasimuliwa kwamba kutokana na hatari za bahari, Waarabu walikuwa wakiagua kwa mganga kama safari haina kisirani kabla ya kuondoka. Wakati mwingine, walimkata kichwa mtumwa (walimuua) ili kutoa sadaka kwa mashetani wa baharini ili kutatua hatari au changamoto mbalimbali kama vile kufanya jahazi liende au kuzamisha chombo cha maadui (Waingereza). Humo baharini katika hayo majahazi watumwa waliumwa, walidhoofu, walifungwa pingu za miguu, minyororo na keekee za chuma shingoni, hakukuwa na matibabu yoyote, walikuwa uchi na walipigwa na baridi na kudhalilika. Halikadhalika, inasimuliwa kwamba Mwingereza alipokuwa anawaokoa watumwa katika majahazi ya Waarabu, alistaajabu na kusikitishwa na hali alizowakuta nazo watumwa kwenye majahazi hayo. “Watumwa walikuwa wamesongana, wanaumizwa shingo zao kwa ajili ya ile miti mibaya waliyofungiwa” (uk. 34). Watumwa wengine walikuwa wamelaliana, wengine wagonjwa na wengine wamekufa wakiwa na miti yao shingoni (uk. 36). Kama ilivyoelezwa hapo juu, maandiko kuhusu utumwa yanaeleza kwamba misafara ya watumwa ilikumbwa na misukosuko na taabu mbalimbali. Hivyo, bahari inawakilisha ukatili wa utumwa (Baderoon, 2009), hatari na mateso mbalimbali waliyokutana nayo watumwa.

**4.4 Bahari Inawakilisha Kifo**

Mbali na hatari, misukosuko na mateso, katika riwaya hii bahari inabeba taswira inayowakilisha kifo. Vifo hivyo vilitokea kwa watumwa na hata wamiliki wao wakiwa safarini, baharini. Inasimuliwa kwamba katika msafara, watumwa wengi walinuia kutoroka kwa kila namna si tu kwa sababu ya kukataa kuwa watumwa huko Bara Arabu bali kutokana na ugumu wa safari yenyewe ya baharini, ikiwamo kifo. Mtipia akizungumza na watumwa wenzake anasema, “Mimi nitatoroka usiku huu. Ni radhi kuuzwa mtumwa katika nchi yetu, lakini sikubali kuvuka bahari…” Watumwa wote walinuia kutoroka na Mtipia, nao wakasema “Heri tuliwe na mafisi magengeni, kuliko kuvuka bahari ya kifo kitupu!” (kur. 28-29). Ni wazi kwamba bahari inawakilisha kifo. Vifo hivyo vilitokana na sababu mbalimbali. Miongoni mwa sababu hizo ni kuharibika kwa vyombo vya usafiri wakati wa safari kama vile matanga ya majahazi kupasuka, milingoti ya majahazi kuvunjika, maji kuingia majahazini na, hatimaye, kuzama na maiti na vitu mbalimbali kuonekana pwani ufukoni. Sababu nyingine ni hali mbaya ya hewa kama vile upepo mkali, mvua nyingi na mawimbi makubwa ya bahari. Hali hiyo ilisababisha matanga kutota maji na kupasuka, majahazi kuzama na wasafiri kufa. Mathalani, kutokana na hali mbaya ya hewa inasimuliwa na msimulizi kwamba, “Ah! Maskini watumwa! …Jahazi lilizama. Waarabu waliogelea kujaribu kujiokoa, lakini walishindwa. Wote walikufa maji” (uk. 31). Aidha, inasimuliwa kwamba mbali na vifo vya baharini “Wako waliovuka salama, walikwenda kufia mbele kwa kufanya kazi nzito” (uk. 31). Wakiwa safarini walimwomba Mungu sana awaokoe kutokana na hali mbaya ya hali ya hewa iliyokuwapo baharini ili vyombo vyao visizame na kusababisha vifo. Suala la kumuomba Mungu ili kuepukana na kifo linatokana na imani kwamba

Mungu ndiye darajia ya juu kabisa katika ontolojia ya kidini ya Kiafrika. Mungu ndiye muumba wa kila kitu na chanzo cha vitu vyote duniani, na ndiye anayewezesha uhai wa vitu vyote (Tempels, 1959; Mbiti, 2011).

Waingereza walichangia kwa kiasi kikubwa kupiga vita biashara ya watumwa katika Bahari ya Hindi na Atlantiki kupitia mikataba ya kisheria ili kufuta na kuzuia biashara hiyo au kwa kutumia doria na mbinu za kijeshi kwa kukamata meli na majahazi yaliyokuwa yanasafirisha watumwa (Sheriff, 1987; Campbell, 2012; Pargas na Schiel, 2023). Hivyo, watumwa wengine walikufa katika hekaheka ya Mwarabu kumkimbia Mwingereza. Mwarabu akiona manowari za Mwingereza alikuwa anawalazimisha watumwa kushuka majini ili wakimbie. Matokeo yake baadhi yao walizama kwa kushindwa kuogelea kutokana na kuwa wamefungwa keekee za chuma shingoni. Pia, watumwa wengine waliuawa baharini kama adhabu kwao pale walipotenda makosa mbalimbali na wengine walitolewa kama kafara au sadaka kwa kukatwa vichwa na kupewa mashetani waliomo baharini ili wafanikishe chombo au safari yao iende salama au ikizamishe chombo cha adui (Mwingereza). Kwa mfano, inasimuliwa katika riwaya kwamba, "Mwinyi Upate alimfungua mtumwa mmoja, akamtoa sadaka kwa kumkata kichwa!" (uk. 33). Ni dhahiri kwamba wamiliki wa watumwa hawakuona uchungu kupoteza uhai wa mtu. Kwa ujumla, biashara ya watumwa ilisababisha watumwa wengi kufa wakiwa njiani kutokana na magonjwa, njaa, mateso, kurushwa baharini, hali mbaya za safari, ukatili wa mabaharia na ukosefu wa matibabu (Sheriff, 1987; Rediker 2007; Campbell, 2012).

Watumwa waliokufa baharini 'walizikwa' humo. Mathalani, inasimuliwa kwamba Waingereza walipowaokoa watumwa (mateka) kutoka majahazi ya Waarabu mle baharini, "waliwachukua wale maiti, wakawatia katika bao moja na wakayatelemsha majini kwa utaratibu wote. Hao mateka waliona hayo mazishi kwa macho yao wenyewe" (uk. 37). Maneno 'kuona mazishi kwa macho yao wenyewe' yakifanyika baharini, kwa kutumia Nadharia ya Udenguzi inayosisitiza kutoa fasiri ya kina ya matini, yanakazia taswira kwamba bahari inaashiria kifo na maumivu makubwa ambayo watumwa walipata. Mbali na watumwa, baadhi ya wamiliki wa watumwa (Waarabu) walikufa baharini humo wakati wa doria iliyofanywa na Waingereza katika kuwakomboa watumwa.

### 4.5 Bahari ni Tumaini la Ukombozi na Uhuru

Mbali na bahari kuashiria kuelekea utumwani, hatari na kifo pia inaashiria njia au tumaini la kujikomboa, ukombozi na kuwa huru. Simulizi za watumwa kuhusu kujikomboa wakiwa baharini zinajitokeza zaidi katika simulizi za watumwa za Amerika na Ulaya. Kupitia baharini, watumwa walifanikiwa kutoroka kutoka maeneo ya kitumwa na kwenda katika nchi ambazo hazikuwa zikiruhusu kabisa utumwa. Baadhi ya watumwa waliona ni heri kujitosa baharini ili kuwa huru au 'kupata uhuru wa kiroho' kuliko kuendelea na safari kwenda kuwa mtumwa au kutumikishwa, ingawa wengi walikufa (Morrison, 1987; Sheriff, 1987; Rediker,

2007). Watumwa walikabiliwa na ukatili na, hivyo, waliupinga na kutoroka (Cooper, 1977).

Katika simulizi za watumwa za Afrika Mashariki na Kati, ikiwamo riwaya hii, ukombozi unatokea pia baharini. Watumwa wengi walikombolewa baharini na Mwingereza ambaye katika kipindi hicho alikuwa anapinga vikali biashara ya watumwa na utumwa. Katika riwaya hii watumwa walikombolewa wakiwa baharini kwa kutolewa kutoka katika majahazi ya Waarabu na kuingizwa katika manowari za Mwingereza ambazo zilikuwa kila mahali baharini kwa lengo la kuwakomboa watumwa. "Manowari zao zilitangatanga huku na huku kutafuta na kuwaokoa watumwa waliokuwa katika majahazi ya Waarabu" (uk. 32). Watumwa walivyookolewa Mwingereza aliwafungua "vile vifungo vya kifo, akawatoa katika lile jahazi la mateso akawatia katika zile mashua za raha" (kur. 34-35). "Mateka walifurahiwa zaidi walipoona vile vifungo vimetumbukizwa baharini" (uk. 39).

Ukombozi huu ulipingwa na kulaaniwa sana na Waarabu. Mathalani, inasimuliwa kwamba mle baharini Waarabu walianza "kukiapiza kile chombo cha Waingereza kwa kutaja majina ya majini, pepo, na mtume wao Muhamadi na kuinua hirizi zao juu na kukielekezea kile chombo cha Waingereza, lakini hayo yote hayakufaa " (uk. 33) kwani hatimaye watumwa walikombolewa. Kwa mujibu wa Nadharia ya Udenguzi ambayo inampa msomaji nafasi ya kutoa tafsiri yake kulingana na muktadha, pia kuhusisha na matini nyingine tunaweza kusema kwamba nguvu za kidini, kama vile dua, zilishindwa ili kuonesha uhalali, ulazima na haki ya ukombozi wa watumwa ambao walikuwa katika mateso. Hakuna dini inayotetea mateso, udhalilishaji na ukosefu wa utu na amani kwa viumbe. Vilevile, nguvu za kishirikina (majini, pepo, hirizi, viapo) zilishindwa kwa sababu ukombozi wa watumwa ulitekelezwa kwa nguvu za dola na silaha za kisasa.

Inasimuliwa pia kwamba baada ya watumwa hao kukombolewa, majahazi ya Waarabu yalitiwa moto au kuvunjwavunjwa. Mwingereza anachorwa kama mtu mwema kwa kuwakomboa watumwa. Baada ya kukombolewa na kufunguliwa vifungo vya kifo, walipewa chakula kizuri, nguo na mablanketi kujisitiri. Ni dhahiri kwamba watumwa waliokolewa kutoka utumwa na kifo na kuingizwa katika uhai, faraja, raha na uhuru. Hivyo, bahari inachorwa kuashiria sehemu ya ukombozi, uhuru na matumaini kutoka kwenye hatari, kifo na utumwa. Waliokombolewa "ndio waliojua furaha ya kweli, na raha waliyoipata katika uhuru huo" (uk. 31). Kuhusu Mwingereza kuwakomboa watumwa, Broich (2017) anaeleza kwamba Jeshi la Majini la Uingereza lilichangia sana katika kusitisha biashara ya watumwa katika maeneo ya pwani za Afrika Mashariki, Zanzibar, Oman na India, waliokuwa wanasafirishwa kwenda sehemu mbalimbali duniani.

Hivyo, palipo na hatari, kifo na utumwa pia pana ukombozi, uhuru na matumaini kutokana na changamoto hizo. Bahari inachorwa kuashiria yote haya, kama ambavyo Derrida (1967) anaeleza kwamba mpaka baina ya jozi za maneno zinazokinzana si thabiti na maana zake hukamilishana ili kupata uelewa wa matini husika.

### 4.6 Bahari Inawakilisha Kani Asilia

Bahari ni kitu chenye nguvu asilia ya kimaumbile ambayo ina athari kwa binadamu, hivyo, hana uwezo wa kuidhibiti. Mathalani, inasimuliwa katika riwaya teule kwamba watumwa waliopakiwa katika majahazi walipata misukosuko ya bahari. Watumwa wengi "hawakuthubutu kuyaangalia maji kwa sababu walikuwa wakishikwa na kizunguzungu, wakitapikiana ovyo tu katika majahazi… kina mama mara kwa mara walikuwa wakijitosa baharini, kwa kuwa vichwa vyao havikuwa vizuri" (uk. 30). Hii inaonesha kani ya bahari kwa viumbe, wakiwamo binadamu. Pia, bahari kama kiwakilishi cha kani imejitokeza kupitia shughuli mbalimbali za kiimani zilizokuwa zikifanyika baharini katika kutatua changamoto mbalimbali. Kwa mfano, inasimuliwa kwamba Waarabu walikuwa wanawachinja watumwa wakiwa katika majahazi na kuwatupa baharini kwa lengo la kutoa sadaka kwa mashetani waishio baharini ili wawaepushe na changamoto mbalimbali. Kwa mfano, "Mwinyi Upate alimfungua mtumwa mmoja, akamtoa sadaka kwa kumkata kichwa! Ati alifanya hivi ili hao mashetani waliozuia lile jahazi lisiende, waridhike kwa kuzamisha kile chombo cha Waingereza!" (uk. 33).

Nadharia ya Udenguzi inasisitiza kwamba kazi ya mtu binafsi haijitoshelezi yenyewe, bali ni zao la uhusiano na maandiko mengine, ya kifasihi na yasiyo ya kifasihi (Derrida, 1972). Kwa matukio haya yaliyokuwa yakifanywa na wamiliki wa watumwa, inaonesha kwamba bahari si tu inawakilisha nguvu bali pia ina viumbe visivyoonekana kama vile mashetani ambao nao wana nguvu fulani. Nguvu hiyo inaweza kudhuru au kuokoa. Wataalamu wa masuala ya falsafa na dini za Kiafrika kama vile Tempels (1959) na Mbiti (2011) wanaeleza kwamba vitu asilia kama vile mimea, maji na milima vinawakilisha kani fulani na hutumika na binadamu kwa shughuli za kidini kama vile kutoa sadaka, kufanya kafara na maombi, kwani vina nguvu ya kiungu na vinaashiria makazi ya viumbe visivyoonekana kama vile miungu, mizimu na mashetani. Aidha, akizungumzia jamii za watu wa pwani, hasa Zanzibar, Larsen (2008) anaeleza kwamba Wazanzibari hutambua ulimwengu wa mizimu na majini, hasa kupitia sherehe za kitamaduni na kidini kama vile ngoma za pepo na matambiko. Majini ni viumbe waliotajwa pia katika Kurani, hivyo, imani hizo ni mchanganyiko wa imani za Kiislamu, Kiswahili na Kiafrika. Aidha, kuna aina mbalimbali za mashetani, wale waishio baharini na wale waishio nchi kavu, wale wanaodhuru na wale wanaosaidia kutoa ulinzi.

### 4.7 Bahari ni Ishara ya Uimara wa Dola (la Mwingereza)

Uimara wa dola tunaweza kusema ni uwezo wa nchi au serikali katika kuendesha na kudhibiti mambo yake mbalimbali kwa uthabiti. Katika riwaya inaoneshwa kwamba Mwingereza alikuwa na vyombo vingi vya majini vilivyokuwa vinazunguka sehemu mbalimbali za bahari kukamata majahazi ya Waarabu yaliyobeba watumwa ili kukomesha biashara hiyo haramu. Mwingereza alikuwa na vyombo vikubwa kama vile manowari (meli zenye mizinga na askari wa vita wa majini), mashua za uokozi na jeshi imara la majini lenye mizinga na silaha

zilizoweza kuona mbali vyombo vya wahalifu (Waarabu). Wakati mwingine Waarabu walikuwa wanakataa Mwingereza asipekue au asiingie kwenye majahazi yao kuwaokoa watumwa lakini kutokana na vyombo vyao imara vya uokoaji waliweza kuingia katika majahazi yao. Inasimuliwa katika riwaya teule kwamba kama Mwarabu anakuwa mbishi, Bwana mkubwa wa manowari (Mwingereza) alimwambia maneno mawili ya Kiingereza, "Shut up!" (uk. 34) na kutulia. Pia, inaelezwa kwamba "katika maji makuu ya "Indian Ocean" hizo manowari za Kiingereza zilikuwa zikitawala, zikivizia majahazi hayo ya Waarabu yaliyopakia watumwa.

Kwa Waingereza kuwakomboa watumwa baharini taswira inayopatikana ni uimara wa dola na jeshi lao la majini katika kukabiliana na uhalifu uliokuwa ukiendelea. Kutokana na uimara huo, wakati wa safari, Waarabu walipokuwa wakiona manowari za Mwingereza walikuwa wakikimbia au walikuwa wakiwaambia watumwa kwamba Mwingereza akifika katika majahazi hayo kuwakomboa wawaambie kwamba wao si watumwa. Pia, ili kuepa mkono wa Mwingereza, Waarabu wakiona manowari za Mwingereza walikuwa wanawafungua watumwa minyororo na miti waliyowafunga. "Katika safari hizi za baharini, kila mtu alikuwa anatumia ujanja wake wa kujiponya na huyo Mwingereza" (uk. 39).

Aidha, huko baharini, Mwingereza alipokwisha kuwakomboa watumwa, aliyateketeza majahazi ya Waarabu. Pia, inasimuliwa kwamba katika sikukuu ya Krismasi mateka hawakuwa na hofu ya kukamatwa utumwa, kwa sababu hapo pwani bandarini, manowari ya Mwingereza ilikuwa imestawi yenye mizinga iliyoelekeza pande zote. Kutokana na kuwa na nguvu hiyo, inasimuliwa kwamba watumwa waliamini walikuwa kwenye mikono salama na walikuwa tayari kuwatumikia Waingereza. Tafiti mbalimbali zinaeleza nguvu za Uingereza za kibiashara na kisiasa katika kuzuia utumwa hasa katika Afrika Magharibi na Mashariki. Hayo yalifanyika kupitia mikataba ya kimataifa, na operesheni za kijeshi za baharini ili kuzuia meli zinazosafirisha watumwa, hivyo, kuwezesha kupungua kwa biashara ya watumwa na hatimaye kukoma kabisa (Sheriff, 1987; Rediker, 2007; Campbell, 2012; Pargas na Schiel, 2023).

### 4.8 Bahari ni Ishara ya Kuungana (tena)

Watumwa walikuwa wakitengwa kwa kuuzwa kwa mabwana tofauti au kutiwa utumwani na mabwana tofauti. Mathalani, katika riwaya hii kuna watumwa waliokuwa chini ya Mwinyi Upate, wengine wa Pwanali na wengine wa Mwinyi Rashidi. Kwa kuwa watumwa hawa walitoka sehemu moja, walikuwa wanafahamiana. Akizungumzia watumwa waliokuwa chini ya Mwinyi Rashidi walivyoungana tena na wenzao wa mabwana wengine, mwandishi anaeleza kwamba wale watumwa walipowaona wenzi wao katika chombo cha Mwingereza, walipiga kelele za kutaka waokolewe. Kadhalika, wale waliokuwa chomboni mwa Mwingereza wakaanza kuwaita wenzi wao. Baada ya kuokolewa watumwa wote

wakatiwa ndani ya chombo cha Mwingereza, “nao walifurahiwa kuonana na jamaa zao, ndugu zao, na hata mtu na mkewe. Walipewa muda mrefu kuamkiana na kufanya kelele” (uk. 40). Simulizi za watumwa zinaonesha kwamba hali waipatayo watumwa baada ya kuungana tena, kupitia kutoroka au kukombolewa, haioneshi tu furaha yao bali pia inadokeza kuhusu machungu na mateso ya kihisia waliyopitia katika utengano wa safari yao ya utumwa (Douglass, 1845; Jacobs, 1861). Bahari si tu inawakilisha utengano baina ya wanafamilia au wanajamii kama tulivyoona awali, bali pia muungano wao. Hivyo, utengano na utangamano vinakamilishana ili kujenga taswira ya bahari katika simulizi ya watumwa.

**4.9 Bahari kama Ishara ya Mabadiliko ya Kiutawala**

Historia inaonesha kwamba shabaha ya Waarabu kutoka Oman kuja Afrika Mashariki ilikuwa kupata watumwa na pembe za ndovu. Baadaye Waarabu hao walitawala pwani ya Afrika Mashariki mnamo karne ya 17 na 19. Mwingereza aliyejitokeza kupiga vita biashara ya watumwa, ingawa alilenga kuimarisha ukoloni na kukuza biashara zake, alitawala Afrika Mashariki kuanzia mwishoni mwa karne ya 19. Kufikia nusu ya pili ya karne ya 19, vuguvugu la mapinduzi ya viwanda huko Ulaya na haja ya kuwekeza mitaji lilikuwa limefika Afrika. Tanzania Institute of Education (1996) inaeleza kuwa katika harakati hizo, jambo la awali kabisa lilikuwa kukomesha biashara ya watumwa ili kurahisisha ufikiaji wa malengo hayo matatu, yaani malighafi kwa ajili ya viwanda vyao, masoko kwa ajili ya bidhaa zao za viwandani na kufungua maeneo mapya ya kuwekeza mitaji yao.

Taswira hii ya bahari kuashiria mabadiliko ya kiutawala inapatikana hasa kupitia taswira ya bahari kama ukombozi. Riwaya ya *Uhuru wa Watumwa* inaonesha kwamba watumwa walikuwa wanakombolewa kutoka kwa Waarabu wakiwa baharini. Tunaona kwamba hii si tu inawakilisha ukombozi bali pia inawasilisha mabadiliko kutoka katika enzi ya Mwarabu kuingia enzi ya utawala mwingine, wa Mwingereza. Mwingereza alipokuwa anawaokoa watumwa na kuwatia katika chombo chake aliwafungua “vile vifungo vya kifo, akawatoa katika lile jahazi la mateso akawatia katika zile mashua za raha” (kur. 34-35). Aidha, inasimuliwa kwamba katika sikukuu ya Krismasi iliyofanyika katika manowari mle baharini, iliyojumuisha Waingereza, wafuasi wao na mateka; vifungo vyote vilivyofunguliwa kutoka kwa watumwa vilitumbukizwa baharini.

Hivyo, ukombozi wa watumwa uliofanywa na Mwingereza mle baharini unaashiria na kuwezesha mwanzo wa utawala wao. Kuhusiana na taswira hiyo ya utawala mpya, inasimuliwa kwamba, “Wenyewe wazee wetu hao mateka waliona tofauti ya Mwingereza na Mwarabu katika mema waliyofanyiwa, na mabaya waliyotendewa” (uk. 37). Watumwa (mateka wa baharini) waliokombolewa kutoka kwa Waarabu walipata fursa mbalimbali kutoka kwa Mwingereza ikiwamo kutembelea Uingereza, kujifunza Kiingereza na michezo mbalimbali, kufunzwa kazi za mikono kama vile ushoni, useremala, uhunzi na uashi, kulima kwa kutumia ng’ombe, na kujifunza dini ya Kimasihia (kur. 48-51). Tafiti mbalimbali zinaonesha

kwamba Waingereza (kupitia watawala, wamisionari na wafanyakazi) walifundisha michezo mbalimbali kama vile mpira wa miguu, riadha, na kriketi si tu kama burudani bali kueneza maadili na tamaduni zao na kudumisha utawala wao kwa wanaowatawala (Mählmann, 1988; Fair, 1997). Wakati wa utawala huo tamaduni za Waswahili zilipuuzwa. Miongoni mwa tamaduni hizo ni kuamini katika mizimu (mizuri na mibaya), uchawi na sihiri (kufanya miviga mbalimbali) ili kujilinda wao wenyewe, familia zao na ardhi yao (Nurse na Spear, 1985; Giles, 1989). Aidha, katika utawala wao inasimuliwa katika riwaya kwamba Mwingereza aliwapiga marufuku mateka kucheza ngoma zao za kishenzi, kuamini mambo ya pepo, uchawi na sadaka kwani "Mwenyezi Mungu hafurahishwi na mambo hayo hata kidogo" (uk. 54). Kwa kuzingatia msingi wa Nadharia ya Udenguzi unaompa nafasi msomaji wa matini kujenga maana kwa kuhusisha matini na maandiko mengine, ya kifasihi na yasiyo ya kifasihi (Derrida, 1972), tunatoa hoja kwamba ukombozi wa watumwa uliokuwa unafanywa kule baharini ulikuwa unaashiria pia mabadiliko ya kiutawala. Historia inaonesha kwamba Mwingereza alitawala baadhi ya nchi za Afrika Mashariki (kama vile Kenya na Tanzania), nao watawaliwa walihimizwa kufuata tamaduni za kigeni na kukatazwa kufuata tamaduni na mila zao.

## 5.0 Dhima za Taswira za Bahari

Taswira za bahari katika riwaya ya *Uhuru wa Watumwa* zina dhima kadhaa. Kwanza, taswira za bahari zinasaidia kuonesha athari mbalimbali za biashara ya watumwa walizopata watumwa au jamii ambazo walitoka watumwa hao. Athari hizo ni pamoja na vifo, kusambaratika kwa familia, kupotea kwa mila na utamaduni wa Afrika Mashariki (Kusimba, 2004), umaskini na nyinginezo. Wakati Waarabu wakipata utajiri kwa biashara ya watumwa, wananchi walizama katika umaskini, walisombwa kwenda kutumikishwa bila ya ridhaa yao, na familia kutengana. Taswira hizi zinabainisha jinsi mtumwa/mtu mweusi alivyonyanyaswa, kuvuliwa utu wake na kudhalilishwa (kuchomwa, kufungwa minyororo, kuwa utupu) kwa masilahi ya wageni. Mathalani, Mwafrika mtumwa baada ya kununuliwa na Mwarabu alitiwa alama za kinyama ili akitoroka aweze kujulikana kwa urahisi na mmiliki wake. Watumwa walikatwa masikio, waling'olewa baadhi ya meno, walipigwa chapa ya misumari ya moto matakoni au migongoni, waliwekwa pete kubwa ya chuma katika mdomo wa juu na kadhalika (uk. 40). Athari nyingine ni kupotea kwa nguvukazi kutokana na watu kusafirishwa kwa wingi kutoka Afrika kwenda utumwani, baadhi ya tamaduni za jamii kupotea au kutangamana na za kigeni.

Pili, taswira hizi zinadokeza jinsi watu wa Afrika Mashariki (kupitia utumwa) walivyoshiriki katika maendeleo ya kiuchumi ya sehemu mbalimbali duniani. Kwa mfano, Martin na Ryan (1977) wanakadiria kwamba kati ya mwaka 1780 na 1896, watumwa wapatao 424,100 kutoka Afrika Mashariki walisafirishwa kwa meli kwenda Uarabuni, Iran na India na takriban watumwa 833,000 walibaki katika pwani ya Afrika Mashariki, wakifanya kazi kwenye mashamba makubwa na

katika kaya za tabaka la juu. Naye Sheriff (1987) anaeleza kwamba biashara ya watumwa, karafuu na pembe za ndovu huko Zanzibar, ambayo ilikuwa kituo kikubwa cha biashara hiyo, ilichangia kwa kiasi kikubwa katika uchumi wa dunia kunako karne ya 18 na karne ya 19. Sheriff anabainisha kwamba mwanzoni mwa karne ya 19, biashara ya watumwa katika Afrika Mashariki ilikuwa na jumla ya watumwa kati ya 6,000 hadi 13,000 ambapo sehemu kubwa ya biashara hiyo ilipitia katika Bahari ya Hindi. Pia, mnamo miaka ya 1850, biashara hiyo ilikuwa na kati ya watumwa 14,000 hadi 15,000, na kunako miaka ya 1860 iliongezeka zaidi hadi kufikia watumwa 20,000 (katika Liebst 2023: 499).

Tatu, taswira hizi zinasaidia kujenga kumbukumbu ya utumwa miongoni mwa jamii (Baderoon, 2009). Taswira hizi za bahari zinatupa taarifa ya namna biashara hiyo ilivyokuwa inafanyika na kutoa kumbukumbu nzuri kwa wasomaji. Taswira hizi zinatupa picha ya biashara hiyo kuanzia uendeshaji hadi jitihada za ukomeshaji wake. Halikadhalika, zinasaidia kudokeza kuhusu uhusiano wa ukomeshaji wa biashara ya watumwa na ukoloni, hususan wa Mwingereza katika Afrika Mashariki ambaye baadaye alitawala baadhi ya nchi katika eneo hilo.

Nne, taswira za bahari zinasaidia kujenga vipengele vingine vya simulizi za watumwa (vya kifani na kimaudhui) kama vile dhamira, migogoro, wahusika na kadhalika. Miongoni mwa dhamira zinazopatikana ni kifo, unyanyasaji, unyonyaji, ukoloni, ukosefu wa haki za binadamu na utu, na ukombozi. Henry (2020) anaeleza kuwa masuala kama unyonyaji na vifo vya wahusika katika simulizi za watumwa yanasawiri hali halisi iliyokuwapo katika jamii ya watumwa na biashara ya watumwa. Kwa upande wa wahusika, uhusiano baina ya watumwa na wamiliki ulikuwa wa kiunyanyasaji na kikatili uliosababisha vifo vingi vya watumwa.

Tano, taswira za bahari pia zinasaidia kubainisha mandhari ya tukio husika. Mandhari ni kipengele cha kifani kinachohusu mahali ambapo wahusika huishi au kujenga matendo yao. Mandhari huhusisha mahali, muda, mazingira ya kijamii na jinsi tukio la fasihi linavyotokea. Mahali ni eneo la kijiografia, muda ni kipindi ambacho tukio la fasihi linatokea, na mazingira ya kijamii ni mahali alipo mhusika na matukio katika jamii fulani. Mandhari husaidia kuwasilisha si tu tukio bali pia hisia za wahusika (Sikuomba, 2024). Hivyo, taswira hizi mbalimbali zinasaidia wasomaji kupata mandhari ya biashara ya watumwa kwamba ilikuwa inafanyika katika pwani ya Afrika Mashariki na watumwa walikuwa wanasafirishwa kupitia Bahari ya Hindi. Aidha, biashara hiyo ilifanyika katika kipindi fulani cha kihistoria (kunako karne ya 18 na 19) na ilihusisha watu au watendaji mbalimbali, wakiwamo watumwa (Waafrika), Waarabu (wamiliki na waendeshaji wa biashara) na Waingereza (wakomeshaji wa biashara hiyo).

## 5.0 Hitimisho

Matokeo yamebaini kwamba bahari katika simulizi hii imechorwa kwa namna kuu mbili, bahari ya kawaida na bahari ya kiishara. Baadhi ya taswira hizo zinakinzana lakini zinajengana na kukamilishana, hivyo, kusaidia kujenga simulizi nzima.

Miongoni mwa taswira hizo ni bahari inaashiria usalama pia hatari au kifo, bahari inaashiria uhuru pia utumwa, na bahari inaashiria muungano pia utengano. Kimsingi, taswira za bahari zinabeba dhima mbalimbali, ikiwamo kuonesha athari mbalimbali za biashara ya watumwa, walizopata watumwa au jamii ambazo walitoka watumwa hao. Pia, zinasaidia kubaini mchango wa wana-Afrika Mashariki (kupitia utumwa) katika maendeleo ya uchumi wa sehemu mbalimbali duniani. Halikadhalika, taswira hizo zinasaidia kujenga kumbukumbu ya utumwa na uelewa wa biashara ya watumwa miongoni mwa wanajamii, kuibua hisia kwa msomaji, kubaini dhamira mbalimbali katika riwaya husika na kusawiri mandhari ya matukio ya utumwa. Kupitia taswira mbalimbali za bahari, makala hii inaongeza maarifa zaidi kuhusu biashara ya watumwa katika tafiti za fasihi ya Kiswahili.

**Marejeleo**

Austen, R.A. (1989). The Nineteenth Century Slave Trade from East Africa (Swahili and Red Sea Coasts): A Tentative Census. *Slavery and Abolition*. 9(3): 21–44.

Baderoon, G. (2009). The African Oceans—Tracing the Sea as Memory of Slavery in South African Literature and Culture. *Research in African Literatures*. 40(4): 89–107.

Beach, A.R. (2013). African Slaves, English Slave Narratives, and Early Modern Morocco. *Eighteenth-Century Studies*. 46(3): 333–348.

Broich, J. (2017). *Squadron: Ending the African Slave Trade*. New York: Overlook Dockworth.

Campbell, G. (Ed.) (2012). *Abolition and its Aftermath in Indian Ocean Africa and Asia*. London: Routledge.

Cooper, F. (1977). *Plantation Slavery on the East African Coast*. London: Yale University Press.

Derrida. J. (1967). *Of Grammatology* (Kimetafsiriwa na Gayatri C. Spivak, 1997). Baltimore: John Hopkins University Press.

Derrida. J. (1972). *Margins of Philosophy* (Kimetafsiriwa na Alan Bass, 1982). Chicago: The University of Chicago Press.

Derrida. J. (1972). *Dissemination* (Kimetafsiriwa na Barbara Jonhson, 1981). Chicago: The University of Chicago Press.

Douglass, F. (1845). *Narrative of the Life of Frederick Douglass, an American Slave, Written by Himself.* Boston: Anti-Slavery Office.

Equiano, O. (1789). *The Interesting Narrative of the Life of Olaudah Equiano or Gustavus Vassa: The African*. London: Hogarth Blake Ltd.

Fair, L. (1997). Kickin' It: Leisure, Politics and Football in Colonial Zanzibar, 1900s-1950s. *Africa: Journal of the International African Institute*. 67(2):224–251.

Giles, L. (1989). Spirit Possession on the Swahili Coast: Peripheral Cults of Primary Texts. Tasnifu ya Uzamivu (Haijachapishwa). University of Texas.

Gilroy, P. (1993). *The Black Atlantic: Modernity and Double Consciousness*. Cambridge: Harvard University Press.

Henry, G. (2020). Uchambuzi Linganishi wa Ujumi wa Kifasihi katika Simulizi Teule za Watumwa kutoka Afrika, Amerika na Ulaya. Tazmili ya Uzamivu (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Jacobs, H.A. (1861). *Incidents in the Life of a Slave Girl.* Boston: Published for the Author.

Khamis, S.A.M. (2005). Signs of New Features in the Swahili Novel. *Research in African Literatures*. 36(1): 91–108.

Kusimba, C.M. (2004). Archaeology of Slavery in East Africa. *The African Archaeological Review*. 21(2): 59–88.

Larsen, K. (2008). *Where Humans and Spirits Meet: The Politics of Rituals and Identified Spirits in Zanzibar*. New York: Berghahn Books.

Liebst, M. (2023). Urban East African Slavery. Katika D.A. Pargas and J. Schiel (Wah.), *The Palgrave Handbook of Global Slavery throughout History*. Macmillan: Palgrave. Kur. 497-516.

Lovejoy, P. E. (1989). The Impact of the Atlantic Slave Trade on Africa: A Review of the Literature. *The Journal of African History*. 30(3): 365–394.

Lovejoy, P.E. (2000). *Transformations in Slavery: A History of Slavery in Africa* (2nd ed.). Cambridge: Cambridge University Press.

Mählmann, P. (1988). Sport as a Weapon of Colonialism in Kenya: A Review of the Literature. *Transafrican Journal of History*. 17: 152–171.

Martin, E.B. na Ryan, T.C.I. (1977). A Quantitative Assessment of the Arab Slave Trade of East Africa. *Kenya Historical Review*. 5: 71–91.

Mbiti, J. (2011). *African Religions and Philosophy*. Nairobi: East African Educational Publishers Ltd.

Mbotela, J. (1934). *Uhuru wa Watumwa*. Nairobi: Nelson.

McLaren, J. (2016). Review: Metaphor and the Slave Trade in West African Literature by Laura T. Murphy. *Journal of West African History*. 2(1): 195–198.

Morrison, T. (1987). *Beloved*. New York: Alfred A. Knopf.

Mulokozi, M.M. (2017). *Utangulizi wa Fasihi ya Kiswahili*. Dar es Salaam: KAUTTU.

Murphy, L.T. (2012). *Metaphor and the Slave Trade in West African Literature*. Athens: Ohio University Press.

Njogu K. na Chimerah, R. (1999). *Ufundishaji wa Fasihi: Nadharia na Mbinu*. Nairobi: Twaweza Communication.

Nurse, D. na Spear, T. (1985). *The Swahili: Reconstructing the History and Language of an African Society, 800-1500*. Philadelphia: University of Pennsylvania Press.

Pargas, D. A. na Schiel, J. (Wah.). (2023). *The Palgrave Handbook of Global Slavery throughout History*. Palgrave Macmillan.

Patterson, O. (1982). *Slavery and Social Death: A Comparative Study*. Cambridge: Harvard University Press.

Rediker, M. (2007). *The Slave Ship: A Human History*. Penguin Books.

Semzaba, E. (1984). *Tendehogo*. Dar es Salaam: Tanzania Publishing House.

Sheriff, A. (1987). *Slaves, Spices and Ivory in Zanzibar: Integration of an East African Commercial Empire into the World Economy*, 1770–1873. London: James Currey.

Sikuomba, B. (2024). Uchunguzi wa Mandhari na Ujenzi wa Wahusika katika Ushairi wa Kiswahili: Mifano kutoka Kazi Teule za Muhammed Seif Khatib. Tasnifu ya Uzamivu (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Tempels, P. (1959). *Bantu Philosophy*. Paris: Presence Africaine.

Thiebaut, R. (2025). Slave Trade in Indian Ocean Africa. *Oxford Research Encyclopedia of African History*. https://doi.org/10.1093/acrefore/9780190277734.013.835

Tanzania Institute of Education (1996). *The Development of African Societies up to the Nineteenth Century*. Dar es Salaam: Dar es Salaam University Press.

Wamitila, K.W. (2008). *Kanzi ya Fasihi: Misingi ya Uchanganuzi wa Fasihi*. Nairobi: Vide~Muwa Publishers Limited.

Wright, M. (1993). Mama Meli: From Slavery to Freedom. *Strategies of Slaves & Women: Life-Stories from East/Central Africa*. New York: Lilian Barber Press. Kur. 91-121.